



Pindi nilipopandishwa juu mbinguni, nilipita kwa watu wakiwa na kucha za shaba, wakizikwarua kwazo nyuso zao na vifua vyao

Imepokelewa kutoka kwa Anas radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake amesema:

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu -rehema na amani ziwe juu yake: "Pindi
nilipopandishwa juu mbinguni, nilipita kwa watu wakiwa na kucha za shaba,
wakizikwarua kwazo nyuso zao na vifua vyao, nikasema: Ni akina nani hao ewe Jibrili,
akasema: Hawa ni wale wanaokula nyama za watu, na wanajitumbukiza katika kuvunja
heshima za watu".

[Ni nzuri] [Imepokelewa na Abuu Daud - Imepokelewa na Ahmad]

Ameeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake: Ya kwamba yeye pindi alipopandishwa juu
mbinguni usiku Israa na Miiraji (safari ya usiku na kupandishwa), alipita kwa watu wakiwa na
kucha za shaba wakizikwarua na kuzichana kwazo nyuso zao na vifua vyao, akamuuliza
rehema na amani ziwe juu yake Jibril amani iwe juu yake: Ni kitu gani walifanya hawa mpaka
wanalipwa kwa adhabu hii? Akasema Jibril amani iwe juu yake: Hawa ni wale wanaosengenya
watu, na wanazungumza vibaya kuhusu heshima zao pasina haki.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/4229>